# RIPOTI YA UNEP YA KUKABILIANA NA PENGO LA UZALISHAJI WA GESI CHAFU YA MWAKA WA 2022, UJUMBE MUHIMU UNAOWASILISHWA

Mabadiliko ya tabianchi ni pigo kubwa kwa wanadamu, kama ilivyodhihirika katika mwaka wa 2022: hasa kupitia mafuriko makubwa yaliyoshuhudiwa katika sehemu kubwa ya Pakistan. Ili kuepuka athari kuwa mbaya zaidi, jamii ya kimataifa ni sharti ipunguze kwa haraka uzalishaji wa gesi chafu. Hata hivyo, toleo la mwaka wa 2022 la *Ripoti ya UNEP ya Kukabiliana Na Pengo la Uzalishaji wa Gesi Chafu: Hatua Ndogo – Mwendo wa Konokono – Kukosa kushughulikia mazingira ni kuhatarisha dunia* inaonyesha kwamba, dunia sharti iimarishe juhudi za kukabiliana na athari zilizopo za mabadiliko ya tabianchi kwa dharura na zile zitakazojiri baadaye. Hata hivyo juhudi za kimataifa za upangaji, ufadhili na utekelezaji wa kukabiliana na pengo hazilingani na hatari zinazoongezeka.

**Hatari za mabadiliko ya tabianchi zinaongezeka kadri ongezeko la joto duniani linavyozidi kuongezeka. Udhibiti na ukabilianaji mkubwa ni muhimu ili kusaidia nchi na jamii zilizo hatarini kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.**

- Ukame wa miaka mingi katika Pembe ya Afrika, mafuriko yasiyotarajiwa Asia Kusini na joto kali la majira ya kiangazi kaskazini mwa dunia ni hatari kwa mazingira, yanatokea kiwango cha nyuzijoto 1.1 tu zaidi ya halijoto ya kabla ya viwanda.
- Ahadi Zinazotolewa na Taifa (NDCs) chini ya Mkataba wa Paris zinakisia ongezeko la joto duniani litafikia kati ya nyuzijoto 2.4 na 2.6 kufikia mwishoni mwa karne hii. Sera zilizopo kwa sasa, hata hivyo zinakadiria ongezeko la nyuzijoto 2.8.
- Kulingana na Ripoti ya 6 ya Tathmini ya Kikundi Kazi cha II cha Jopo la Serikali Mbalimbali Kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (IPCC), dunia inakabiliwa na hatari za mabadiliko ya tabianchi zitakazoongezeka kutokana na kuongezeka kwa kila sehemu ya digrii.
- Kukabiliana na hali hiyo ni lazima tuchukue hatua muhimu, ikijumuisha kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi duniani. Hata hivyo, hata uwekezaji kabambe katika kukabiliana na hali hii hauwezi kuzuia kikamilifu athari za mabadiliko ya tabianchi, na kwa hivyo hasara na uharibifu lazima vishughulikiwe ipasavyo.

**Zaidi ya nchi nane kati ya kumi sasa zina angalau chombo kimoja cha kupanga mikakati ya kitaifa, na zinaendelea kuwa bora na jumuishi zaidi.**

- Angalau asilimia 84 ya Wanachama wa Mkataba wa Mfumo wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (UNFCCC), ongezeko la asilimia 5 ikilinganishwa na mwaka jana, wameanzisha mipango, mikakati, sheria na sera za kukabiliana na hali. Takriban nusu yao wana zaidi ya chombo kimoja cha kuweka mikakati.
- Theluthi moja ya Nchi 197 Wanachama wa UNFCCC wamejumuisha malengo yaliyowekewa muda maalum, ambayo ni sehemu inayoongezeka ya mikakati ya ukabilianaji wa kitaifa.

- Takriban asilimia 90 ya zana za upangaji zilizochanganuliwa zilijimuisha jinsia na/au makundi yaliyotengwa kihistoria, kama vile watu wa kiasili.

**Lakini, ufadhili wa kuwezesha mipango na mikakati hii kutimia bado hautiliwi maanani. Usambasaji wa fedha za kukabiliana na hali katika nchi zinazoendelea ni mara 5 hadi 10 chini ya makadirio yanayohitajika na pengo linaendelea kupanuka.**

- Usambasaji wa fedha za kukabiliana na hali katika nchi zinazoendelea unaongezeka polepole. Ulifikia dola bilioni 29 mwaka wa 2020, kama ilivyoripotiwa na nchi wafadhili, ongezeko la asilimia 4 ikilinganishwa na mwaka wa 2019, ikiwa ni asilimia 34 ya jumla ya fedha za kushughulikia hali ya hewa.
- Usambasaji wa fedha za kukabiliana na hali katika mwaka wa 2020 ulipungua kwa angalau dola bilioni 17 ukipungua na dola bilioni 100 zilizoahidiwa kutolewa kwa nchi zinazoendelea. Uharakishaji mkubwa unahitajika ikiwa kuongezeka maradufu kwa usambasaji wa fedha wa mwaka wa 2019 kufikia mwaka wa 2025 kutafikiwa, kama ilivyohimizwa na Mkataba wa Hali ya Hewa wa Glasgow, uliopitishwa kwenye COP26 katika mwaka wa 2021.
- Makadirio ya mahitaji ya kila mwaka ya kukabiliana na hali ni dola za Marekani kati ya bilioni 160 na bilioni 340 kufikia mwaka wa 2030 na dola za Marekani kati ya bilioni 315 na bilioni 565 kufikia mwaka wa 2050.

**Utekelezaji wa hatua za kukabiliana na hali hiyo unaongezeka lakini hauendani na athari za mabadiliko ya tabianchi.**

- Idadi na kiwango cha hatua za kukabiliana na hali hiyo zinazoungwa mkono kupitia ufadhili wa mazingira wa kimataifa, ufadhili wa kimataifa, na msaada kutoka kwa wafadhili kutoka nchi mbili unaendelea kuongezeka.
- Hatua zimejikita katika kilimo, maji, mifumo ya ekolojia na sekta anuai. Kimsingi zinashughulikia ukame, mafuriko na kutofautiana kwa majira ya mvua.
- Hata hivyo, bila kuimarisha ufadhili, hatua za kukabiliana na hali hiyo zinaweza kuzidiwa na madhara yanayoongeza ya mabadiliko ya tabianchi, ambayo yatapanua zaidi pengo la hatua za kukabiliana na hali.
- Hatua za sasa za kukabiliana na hali hazifikii kile kinachohitajika, lakini kuna uelewa mzuri kuhusu jinsi ya kuziboresha.

**Kwa kuzingatia uhusiano kati ya juhudi za kudhibiti na kukabiliana na athari kuanzia kwa kuweka mikakati, ufadhili, na utekelezaji kunaweza kuongeza manufaa ya kushirikiana.**

- Ukabilianaji zaidi utahitajika, na hasara na uharibifu zaidi utatokea, ikiwa upunguzaji hautatosha. Hii inafanya upunguzaji na ukabilianaji kuingiliana kihalisi.
- Kuzingatia kukabiliana na kupunguza athari kuanzia kwa kuweka mikakati, ufadhili, na utekelezaji kunaweza kuongeza manufaa na kupunguza hatari, kama vile nishati ya maji kupunguza utoshelezaji wa chakula au unyunyuziaji maji mimea kuongeza matumizi ya nishati.
- Baadhi ya masuluhisho ya tabianchi hupunguza madhara ya mabadiliko ya tabianchi na huchangia kukabiliana na hali hiyo: hasa masulisho kutokana na mazingira kama vile kupanda na kuhifadhi mikoko, kurejesha mabwawa ya chumvi au kutunza maeneo ya mboji.

**Kujitolea kikamilifu kisiasa kunahitajika ili kuimarisha uwekezaji na matokeo yake.**

- Vita nchini Ukrainia, uhaba wa usambasaji wa bidhaa duniani na janga la COVID-19 vyote vimechangia kwa kuongezeka kwa tatizo la nishati na utoshelezaji wa chakula,

huku gharama za maisha pamoja na mfumuko wa bei ukiongezeka katika nchi nyingi duniani.

- Hata hivyo, majanga haya hayawezi kuruhusiwa kutatiza juhudi za kimataifa za kuimarisha ukabilianaji wa hali. Utashi wa kisiasa ambao haujawahi kushuhudiwa na uwekezaji wa muda mrefu zaidi wa kukabiliana na hali unahitajika kwa haraka ili kukomesha kupanuka kwa pengo la kukabiliana na hali hiyo.
- Mataifa lazima yaunge mkono maneno makali katika Mkataba wa Hali ya Hewa wa Glasgow kwa kuchukua hatua dhabiti za kukabiliana na kupunguza hali na hasara na uharibifu, kuanzia COP27 mjini Sharm El-Sheikh, nchini Misri.